

JINA ..... TAREHE .....

NAMBA YAKO ..... SAHIHI .....

102/2

KISWAHILI: LUGHA

(Ufahamu, Ufupisho, Matumizi ya Lugha na Isimu Jamii)

KARATASI YA 2

JULAI /AGOSTI, 2014

MUDA: SAA 2½

## MTIHANI WA PAMOJA WA SHULE ZA UPILI WILAYANI MAKINDU, 2014

*Kenya Certificate of Secondary Education (K.C.S.E)*

### MAAGIZO KWA MTAHINIWA

Jibu maswali yote.

Majibu yote yaandikwe katika nafasi zilizoachwa katika kijitabu hiki cha maswali.

Karatasi hii ina kurasa nane. Watahiniwa ni lazima waangalie kama kurasa zote za karatasi hii zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo

### KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE

SWALI	UPEO	ALAMAMA
1	15	
2	15	
3	40	
4	10	
JUMLA	80	

## 1. UFAHAMU

### Soma makalama yafuatayo kisha ujibu maswali.

Nimekaa na kutafakari kwa kipindi kirefu, juu ya mabilioni ya pesa ambayo yametengwa na serikali ili kudhamini miradi ya maendeleo ya wanawake. Kina mama au wanawake wengi wanakiri na kusema kwamba fedha hizo zimewezesha kuwaondoa katika lindi la unyanyasaji kutoka kwa waume zao. Kwani kila mmoja anamheshimu mwenzake kwa sababu ya kipato alichonacho. Wengi wameweza kuanza biashara ndogondogo ambazo huwaletea angaa kipato kidogo.

Ukweli ni kwamba fedha hizi zimesaidia kuwatoa wanawake wengi katika unyanyasaji, kwani wengi wanaweza kuanzisha kazi za ujasiriamali na hata kuendesha shughuli mbalimbali za maendeleo.

Kutokana na mafanikio haya, wabunge waliopitisha hoja bungeni za kuanzisha mpango huu wa kuwakwamua wanawake kimaendeleo wanafaa kupongezwa. Mafanikio haya yamewafanya akina mama kujikimu kimaisha na hivyo kutowategemea wanaume katika kila jambo.

Ukitaka kujua ukweli kuhusu hili, nenda kwenye masoko utaona akina mama jinsi wanavyohangaika na biashara zao. Kwa hivyo, ujasiriamali huendelezwa na akina mama zaidi na hivyo wanapaswa kuwezesha kwa hali na mali.

Akina mama pia wanafaa kupongezwa kwani wameamua kujitosa kukopa fedha kutoka kwenye taasisi mbalimbali za fedha. Fedha hizo kwa kiwango kikubwa zimewainua kutoka katika ufukara uliokithiri hadi katika maisha ya heshima. Wale ambao hawajajaribu kuchukua mikopo, ni muhimu wafanye hivyo ili wajikimu kimaisha.

Maisha ya sasa ni magumu, hivyo yanahitaji kusaidiana kwa kila hali na mali. Wanaume kwa wanawake ni vyema wachange bia ili wazumbue riziki. Ushirikiano utarahisisha maisha yao. Hata hivyo, sio tu akina mama hao wameondokewa na unyanyasaji waliokuwa wakiupata ndani ya nyumba zao, toka kwa akina baba, bali hata masualama ya mrundikano wa kesi za kugombea ardhi kwa akina mama, zimepungua. Sababu ni kwamba akina mama wengi wameweza kujitafutia ardhi wenyewe kwa fedha walizonazo.

Ukweli ni kwamba hali imebadilika. Kinyume na hapo awali, ambapo majumba ya kifahari na mashangini yalikuwa hifadhi ya wanaume, siku hizi wanawake wanamiliki hayo yote.

### **Maswali**

1. Taja dhamira mbili za makalama haya.

(alama 2)

.....  
 .....

2. Eleza ni kwa nini msimulizi anawapongeza wabunge

(alama 2)

.....

.....

.....

3. Wanaume walikuwa wakirudisha nyuma maendeleo nchini kivipi?

(alama 2)

.....

.....

.....

4. Sera za serikali zimesaidia wanawake kivipi?

(alama 3)

.....

.....

.....

5. Eleza kwa nini baadhi ya wanawake wanaishi katika lindi la umaskini kulingana na makalama haya.

(alama 3)

.....

.....

.....

6. Eleza maana ya msamiati na mafungu yafuatayo kama yalivyotumika katika makalama haya

(alama 3)

a) Kutafakari

.....

.....

.....

b) Kuwaondoa katika lindi la unyanyasaji

.....

.....

.....

c) Riziki

.....

.....

.....

## 2. UFUPISHO

Katika karne hii na ya kesho, urafiki ni ngome kuu duniani ambayo huhifadhi maslahi ya kila rafiki. Rafiki mwema humpenda mwenzake si kwa sababu ni tajiri ama ana cheo kikuu nchini. Rafiki mwadilifu huridhika na hali aliyonayo rafikiye; akiwa tajiri au maskini, ana cheo, hana. Rafiki mwema huwa mwadilifu wakati wowote. Wakati wa neema hushirikiana na rafikiye katika furaha na wakati wa shida hushirikiana naye katika huzuni na taabu zote zinazomkabili.

Sahibu mwema hutoa alichonacho kumkomboa rafiki yake, huwa radhi kabisa kufilisika kwa ajali yake. Mahali pa finyo hujasiri kuingia ili kumkomboa rafiki yake, hushughulika zaidi kuliko wana ndugu wa toka nitoke. Kwa vyovyote hula naye tamu na chungu pamoja, mkono kwa mkono katika maisha yao yote hadi mmoja wao akaitoka dunia. Urafiki wa namna hii ndio uletao baraka ya Mungu, kuwashukia viumbe hao kama umande wa asubuhi.

Urafiki ni lazima sana katika maisha ya wanadamu. Urafiki ni mfano wa mishipa ipitishayo damu mwilini ili kurutubisha kila sehemu ya mwili. Ingawa ni bora kuwa na marafiki wengi lakini kila marafiki wanapozidi, ni hatari kuangukia kwenye marafiki wadanganyifu-hasidi. Pasi na shaka, ni heri maadui kuliko marafiki wadanganyifu. Hivyo basi tukiwa na rafiki walio kinyume cha wema na upole wa kulinda haki za wanadamu na wasiomcha Mungu ni lazima tuwaepuke. Ingawa ni hivyo vile vile sheria inatukataza tuisikilize na kujali ubaya wa mtu yeyote pasipo kuhakikisha. Huenda ikawa ni uvumi tu usiokuwa na msingi wowote. Ikiwa rafiki ni mbaya, hakosi atajulikana kwani mtungi mbovu haukawii kuvunjika. Lazima tuwapende watu wote ili kutimiza haki za kibinadamu na kuchukuia matendo maovu. Rafiki waovu si vema kuwaacha katika maangamizi ya ubaya wao bali ni lazima tuwaambie waziwazi ili wapate kuongoka. Ukimsamehe rafiki, unaponya donda lake moyoni. Hivyo ni bora kuliko kumtazama na hali anazidi kukosa.

### Maswali

- a) Kwa maneno yasiyozidi 60, fupisha aya ya kwanza na ya pili. (alama 7)

### Nakalama chafu

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

### Nakalama safi

.....

.....

.....

.....

.....

- b) Ni muhimu kuwa na rafiki na marafiki na kuwachagua kwa umakinifu. Kwa kurejelea aya ya tatu, thibitisha kauli hii. (maneno kati ya 50-55) (alama 5)

**Nakalama chafu**

**Nakalama safi**

**3. MATUMIZI YA LUGHA (Alama 40)**

1. Tungia neno lifuatalo sentensi (alama 1)  
Wa'lakini

2. Taja sifa tatu za sauti ifuatayo (alama 3)  
|th|

3. Onyesha mzizi katika neno machweo

(alama 2)

4. Andika katika ukubwa

(alama 2)

Mke wa mzee huyu hupenda watoto sana.

5. Fakinisha

(alama 2)

Kama Otoyo haji mwalimu hatasahihisha kazi.

6. Tunga sentensi sahili mbili kubainisha matumizi mawilitofauti ya 'po'

(alama 2)

7. Eleza matumizi mawili ya koloni na utoe mfano kwa kutunga sentensi

(alama 2)

8. Unda nomino mbili kutokana na kitenzi kinai

(alama 2)

9. Tunga sentensi kudhihirisha ngeli ya KU-

(alama 1)

10. Bainisha yambwa katika sentensi ifuatayo

(alama 2)

Askofu aliandikiwa barua na waumini

11. Bainisha virai katika sentensi

(alama 2)

Chake chote kilivunjika vibaya sana.

12. Changanua kwa matawi

(alama 4)

Ibada ya wafu iliyofanyika jana usiku ilisababisha kilio kingi.

For More Free KCSE Past papers Visit [www.freekcsepastpapers.com](http://www.freekcsepastpapers.com)

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

13. Tunga sentensi moja kutofautisha ‘thibiti’ na ‘dhibiti’ (alama 2)

.....

.....

14. Andika katika usemi wa taarifa (alama 2)

“Aisee! yale mawimbi ya tsunami yaliangamiza biashara nyingi sana” alisema Koinange.

.....

.....

.....

15. (alama 1)

i) Mofimu ni nini? (alama 1)

.....

.....

ii) Taja aina mbili za mofimu na kwa kila aina utoe mfano. (alama 2)

.....

.....

.....

16. Andika katika hali ya mazoea kwa kutumia kirejeshi mwafaka (alama 2)

Mtoto ambaye hula lishe bora ndiye hukua nyema.

.....

.....

.....

17. Andika kinyume (alama 2)

Wanaskauti wengi walivunja kambi jana asubuhi.

.....

.....

.....

18. Tunga kitenzi kishirikishi kipungufu sentensi. (alama 1)

.....

.....

